

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUMBULI



**TANGAZO KWA UMMA KUHUSU MIKOPO
INAYOTOLEWA KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE,
VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU**

(Limetolewa kwa kuzingatia sura ya 290 kifungu cha 37A (4))

Mkurungezi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli anatanganza uwepo wa fedha kwa ajili ya kukopesho vikundi vya wanawake, vijana na watu wenyе ulemavu. Jumla ya shilingi **200,000,000.00** zimetengwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwaajili ya mikopo. Vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuwasilisha maombi katika ofisi za serikali za mitaa ngazi ya Kata zilizopo katika maeneo yenu.

Kikundi kinachoomba mikopo kinapaswa kuwa na viambatisho vifuatavyo; Barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na Afisa Mtendaji wa Kata na Kijiji, Barua ya kikundi kuomba mkopo, Muhstasari wa kikundi wa kuomba mkopo, Andiko la Mradi unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyo ndani ya mfumo na taarifa ya akaunti ya kikundi kutoka benki husika (Bank statement).

Sifa za vikundi vinavyotakiwa kuomba mkopo ni kama zifuatavyo; -


- i) Kiwe ni kikundi cha wanawake, vijana na watu wenyе ulemavu.
- ii) Kiwe kimetambuliwa na Mamlaka za Serikali za Mtaa kupitia Mfumo wa Kieletroniki wa utoaji na usimamizi wa mikopo.
- iii) Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za ujasiriamali au kikundi kinachotarajia kuazisha shughuli za ujasiriamali.

- iv) Kikundi cha wanawake na vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano (05) na kuendelea na kikundi cha watu wenye ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili.
- v) Pia kwa kuzingatia kanuni ya 6a (1) mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenye ulemavu endapo Timmu ya Menejimenti ya Halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa watu wengine wenye ulemavu, na kuungana nao katika eneo lake. Aidha, sifa nyingine zitafanana na sifa za vikundi vingine.
- vi) Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali.
- vii) Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenye akili timamu na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea Aidha, kikundi cha vijana kitapaswa kuwa na wanakikundi wenye umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45.
- viii) Kikundi kisiwe kinadaiwa mkopo na Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli.
- ix) Kikundi kisiwe na wajumbe wenye ajira rasmi.

Maombi yote yatumwe kupitia Mfumo wa kielektroniki (tembelea tovuti mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz) ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasiliana na Afisa Maendeleo ya Jamii wa Kata au Mtendaji wa Kata husika.

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe **15 APRIL 2025**.

Tangazo limetolewa na:-


**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
BUMBULI**

BARAKA M. ZIKATIMU

MKURUGENZI MTENDAJI

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUMBULI.